JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MFUMO WA SERA ZA JUMLA ZA UCHUMI NA MAENDELEO YA JAMII KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2006/07-2008/09



Umetolewa na:

WIZARA YA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI

DAR ES SALAAM-TANZANIA

JUNI, 2005

Mfumo wa Sera za Jumla za Uchumi na Maendeleo ya Jamii Katika Kipindi cha Mwaka 2006/07 – 2008/09

YALIYOMO

Ukurasa

I: MUHTASARI WA MAFANIKIO YA UCHUMI JUMLA 1

II: MAPITIO YA MWENENDO WA UCHUMI JUMLA KATIKA MWAKA 2005/06 NA MTAZAMO WA MUDA WA KATI 4

Ukuaji wa Uchumi 4
Mwenendo wa Bei 8
Mapato na Matumizi ya Serikali 9
Mapato 9
Matumizi 10
Deni la Taifa 11
Ujazi wa Fedha na Karadha 12
Ujazi wa Fedha 12
Mikopo ya Benki za Biashara Katika Sekta Mbalimbali 14
Maendeleo katika Soko la Fedha 14
Soko la Hisa la Dar es Salaam 14
Mwenendo wa Viwango vya Riba 15
Viwango vya Riba kwa Fedha za Kigeni 16
Mikopo Midogo 18
Sekta ya Nje 18
Jumuiya ya Afrika Mashariki 22
Mpango Mpya wa Ushirikiano wa Kuleta Maendeleo Afrika 23
Kujiunga na Mpango wa Afrika wa Kujitathmini na kujipima Zenyewe 23
Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 24
Uwekezaji wa Mitaji ya Kigeni ya Moja kwa Moja 26
Urekebishaji na Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma 27
Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania 28
Umaskini Vijijini 28
Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara 29

III. MASUALA MUHIMU YA KISERA YALIYOJITOKEZA MWAKA 2005/06 30

Ukuaji wa Uchumi 30
Marekebisho ya Sekta ya Umma 31
Maendeleo ya Kilimo 31
Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali 32
Ujazi wa Fedha na Karadha 32
Kuongeza Uwekezaji katika Miundombinu 33
Mazingira 33
Utafiti na Maendeleo 34

Huduma za Kijamii 34
Mpango wa Tanzania wa Kuharakisha Maendeleo 2020 35
Awamu ya Pili ya Mageuzi ya Sekta ya Fedha 36

IV. MISINGI NA MALENGO YA UCHUMI NA MAENDELEO YA JAMII 2006/07-2008/09 36

VI MALENGO NA SHABAHA YA SERA ZA UCHUMI JUMLA KATIKA MWAKA 2006/07 -2008/09 37

V. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI NA UFUATILIAJI WA MASUALA MUHIMU YALIYOJITOKEZA NA MISINGI NA MALENGO YA SERA ZA JUMLA ZA UCHUMI NA MAENDELEO YA JAMII, 2006/07 – 2008/09 38

I: MUHTASARI WA MAFANIKIO YA UCHUMI JUMLA

1. Katika kipindi cha miaka ya karibuni, kumekuwepo na mafanikio makubwa katika mwenendo wa uchumi jumla ambayo yalichangiwa hasa na hatua madhubuti zilizochukuliwa na serikali katika kurekebisha sera na mfumo wa uchumi. Mwaka 2005, Pato Halisi la Taifa liliongezeka kidogo na kufikia asilimia 6.8, kutoka asilimia 6.7 mwaka 2004. Ukiondoa sekta ya kilimo ambayo ukuaji wake ulishuka kidogo kutokana na ukame, ukuaji katika sekta nyingine uliongezeka. Kasi ya upandaji bei ilikuwa asilimia 4.3 mwaka 2005 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2004. Aidha, kuendelea kwa ukame katika robo ya mwisho ya mwaka 2005 ambao uliathiri uzalishaji wa chakula na umeme, sambamba na kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli, kasi ya upandaji bei iliendelea kupanda na kufikia asilimia 6.5 ilipofika Machi, 2006.

2. Mapato ya ndani yamekuwa yakiongezeka na hasa kutokana na kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mapato. Kuongezeka kwa mapato kulitokana pia na kuimarika kwa mfumo wa usimamizi wa ukusanyaji wa kodi. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2005/2006, matumizi ya Serikali yalizidi kiwango kilichopangwa kutokana na kuahirishwa kwa Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2005 na ruzuku iliyotolewa kwenda TANESCO ili kukabili tatizo la umeme.

3. Katika mwaka ulioishia Desemba 2005, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M_3) uliongezeka hadi asilimia 38.0 ikiwa ni kiwango cha juu ikilinganishwa na asilimia 19.3 mwaka 2004. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M_2) uliongezeka kwa asilimia 36.9 ikilinganishwa na asilimia 19.2 Desemba 2004. Ongezeko katika ugavi wa fedha kwa M_2 na M_3 ulitokana hasa na kuongezeka kwa mikopo kwenda sekta binafsi pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya Serikali (kama ilivyoianishwa katika aya ya 2 hapo juu) ambapo ilibidi kuongeza mikopo kutoka Benki.

4. Mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwenda sekta binafsi iliongezeka hadi asilimia 34.4 mwaka ulioishia Desemba, 2005 ikilinganishwa na asilimia 32.9 kipindi kama hicho mwaka uliotangulia. Ongezeko hilo lilichangiwa na: kuongezeka kwa idadi ya wateja wanaokopesheka katika soko la ndani, kuongezeka kwa ushindani katika sekta ya benki, kuwepo kwa mpango maalumu wa kuwadhamini wafanyabiashara wanaouza bidhaa nje ya nchi na juhudi zinazofanywa na serikali za kuboresha mazingira ya biashara nchini. Aidha, tofauti kati ya viwango vya riba ya mikopo na amana bado ni kubwa, hivyo kudhihirisha udhaifu wa kimuundo na mashaka walionayo benki kuhusu uwezo wa wateja kurejesha mikopo.

5. Kutokana na utafiti uliofanywa na Benki Kuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Kituo cha Uwekezaji Tanzania, takwimu za sekta ya nje kwa kipindi cha 2001-2005 zilipitiwa upya, na hivyo kuboresha takwimu za biashara ya nje. Kutokana na mpangilio huo mpya, mwenendo wa sekta ya nje umeonyesha kuwa mwaka 2005 uuzaji nje wa bidhaa asilia na zisizo asilia uliongezeka ambapo thamani ya bidhaa zilizouzwa nje iliongezeka na kufikia dola 1,676.3 milion, ikilinganishwa na dola 1,473.1 milion mwaka2004, sawa na ongezeko la asilimia 13.8. Thamani ya uagizaji bidhaa toka nje iliongezeka kwa asilimia 13.8, kutoka dola 2,339.7 milion mwaka 2004, hadi dola 2,661.8 milion mwaka 2005. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za mitaji na za kati, kufuatia kukua kwa viwanda, uchimbaji madini na shughuli za utalii.

6. Kwa lengo la kuboresha mazingira ya biashara nchini, Serikali iliendelea kukiimarisha Kituo cha Uwekezaji ili kuhamasisha wawekezaji kutoka nje na wa ndani. Aidha, utekelezaji wa Program ya Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA) uliendelea kwa lengo la kujenga mazingira bora na endelevu ya kuendeleza sekta binafsi kwa kuboresha na kuimarisha utawala, taratibu na sheria za biashara. Wakati mchakato wa ubinafsishaji unakaribia kumalizika, Serikali imeanzisha Mawakala wa Udhibiti ambao watasimamia na kuhakiki utendaji wa makampuni yaliyobinafsishwa. Jedwali Na.1 linaonyesha muhtasari wa mwenendo wa baadhi ya viashiria muhimu vya uchumi jumla kwa kipindi cha 1996 – 2005.

Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Mwenendo wa Baadhi ya Viashiria Muhimu vya Uchumi Jumla

	1997	1998	1999	2000	2001	2002	2003	2004	2005[p]
Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa- %	3.3	4	4.7	4.9	5.7	6.2	5.7	6.7	6.8
Kasi ya Upandaji Bei (wastani kwa mwaka) -%	16.1	12.9	7.8	6	5.2	1.0	3.5		4.3
Thamani ya shilingi. (Tshs/USD) –wastani wa mwaka	612.1	664.7	744.8	808.4	876.4	966.6	1038.6	1089.3	1128.8
Thamani ya shilingi. (Tshs/USD) – mwisho wa mwaka	624.6	668	797.3	803.3	916.3	976.3	1063.6	1042.9	1165.5
Mauzo ya Bidhaa Nje (mil. US$) - FOB	752.6	588.5	543.3	663.3	851.3	979.6	1216.1	1473.1	1676.3
Uagizaji wa Bidhaa Toka Nje (mil. US$) - FOB	1148	1382.2	1415.4	1367.6	1560.3	1511.3	1933.5	2339.7	2661.8
Uwiano wa Mauzo ya Bidhaa Nje na Uagizaji %	65.6	42.6	39.7	49.6	54.6	64.8	62.9	63	63
Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho wa Mali (mil. USD)	-403.4	-905.4	-829.5	-498.6	-237.4	22.3	-111	-259.4	-592.7
Uwiano wa Uwekezaji na Pato la Taifa - %	14.7	16	15.4	17.6	17	18.9	18.5	21	17
Uwekezaji wa Moja kwa Maja (FDI) - mil. USD	157.8	172.2	516.7	463.4	467.2	429.8	526.8	469.9	325
Akiba ya Fedha za Kigeni (thamani ya miezi ya uagizaji)	3.8	3	4.1	5.6	6.3	8.6	9.2	8.2	6.4
	1997/98	1998/99	1999/00	2000/01	2001/02	2002/03	2003/04	2004/05	2005/06
Uwiano wa Mapato ya Ndani na Pato la Taifa%	12.6	12.5	11.3	12.2	12.1	12.8	13.4	13.1	14.2[*]
Uwiano wa Matumizi Yote na Pato la Taifa %	17.4	17.6	18.3	20.6	19.1	23.4	24.9	24.4	27.7[*]
Nakisi/Salio katika Mapato na Matumizi ya Serikali (bila misaada) - % of GDPmp	-2.3	-2.3	-5.8	-4.6	-5.6	-8.2	-11.2	-11.8	-13.5[*]
Salio Katika Mapato na Matumizi ya Serikali (ikijumuisha misaada) - % of GDPmp	0.2	0.8	-1.6	-1.2	-1.1	-1.7	-4	-4.5	-6.6[*]
Ukuaji wa Ujazi wa Fedha (M_2) - %	11	11.1	15	12.5	12.3	13	14.2	19.2	36.9[**]
Wastani wa Riba ya Amana - %	10	7.9	7.1	4.2	3.5	3.1	2.4	2.5	3.94[**]
Wastani wa Riba ya Mikopo -%	24	24.5	22.1	19.6	16.4	15. 7	14	14.4	15.24[**]
Mikopo iliyopokelawa Toka Nje(mil. USD)	6435.8	6580.3	6538.3	6312.2	6559.7	6413.4	6730.8	6,99.6	6743.6[*]
Jumla ya Madeni Yote (mil. USD)[2]	7384.6	7669.7	7624.8	7482.1	7464	7268.17	7890.7	9,219.3	9383.9[*]

Chanzo: Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshajii

II: MAPITIO YA MWENENDO WA UCHUMI JUMLA KATIKA MWAKA 2005/06 NA MTAZAMO WA MUDA WA KATI

Ukuaji wa Uchumi

7. Mwaka 2005, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 6.8 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2004. Pato la wastani la kila mtu (kwa bei za miaka husika) lilifikia sh. 379,077 mwaka 2005 kutoka sh. 319,754 mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 18.6. Aidha, Pato la wastani la kila mtu (kwa bei za mwaka 1992) lilikuwa sh. 61,665 ikilinganishwa na sh. 59,335 mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 3.9. Wakati Pato la Taifa lilikuwa kama ilivyochapishwa kwa mwaka 2004, kisekta takwimu zilirekebishwa ipasavyo kama inavyoonyeshwa katika majedwali 2(a) na 2(b).

8. Ukiondoa sekta ya kilimo ambayo ukuaji wake ulishuka kidogo kwa sababau ya ukame uliotokea katika maeneo mengi nchini, viwango vya ukuaji katika sekta nyingine viliongezeka katika mwaka 2005. Ukuaji wa sekta ya kilimo ulipungua kutoka asilimia 5.8 mwaka 2004 hadi asilimia 5.2 mwaka 2005. Kupungua kwa ukuaji wa sekta ya kilimo sambamba na kuongezeka kwa ukuaji wa sekta nyingine, kumesababisha kupungua kwa mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa kutoka asilimia 46.3 mwaka 2004 hadi asilimia 45.6 katika mwaka 2005.

9. Sekta ya madini ilikua kwa asilimia 15.7 mwaka 2005 ikilinganishwa na asilimia 15.4 mwaka 2004. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uwekezaji katika mgodi wa dhahabu wa Tulawaka-Biharamulo. Baada ya kudorora kwa miaka miwili mfululizo katika ukuaji, sekta ya bidhaa za viwandani ilikua kutoka asilimia 8.6 mwaka 2004 hadi asilimia 9.0 mwaka 2005. Ukuaji huo ulichangiwa hasa na kuongezeka kwa uzalishaji wa sementi, sigara, vinywaji na nguo. Ukuaji katika sekta ya ujenzi ulifikia asilimia 11.9 mwaka 2005, kutoka asilimia 10.8 mwaka 2004, ikiashiria kuongezeka kwa uwekezaji katika miundombinu, ikijumuisha barabara na madaraja, majengo ya biashara na makazi, na miradi ya maji. Sekta ya uuzaji wa jumla, rejareja na mahoteli (ikijumuisha utalii) ilikua kwa asilimia 8.2 mwaka 2005 ikilinganishwa na asilimia 7.8 mwaka 2004, kutokana na kuongezaka kwa shughuli za biashara na utalii. Ukuaji katika sekta ya uendeshaji serikali na utawala ilifikia asilimia 5.1, kutoka asilimia 4.3 mwaka 2004, kutokana na kuongezeka na matumizi ya Serikali ili kutekeleza majukumu.

10. Matarajio ya ukuaji wa uchumi katika kipindi cha 2006/07-2008/09 ni kama inavyoianishwa katika majedwali 2(a), 2(b) na 2(c) hapo chini ambayo yanaonyesha mwenendo wa kuridhisha katika ukuaji wa uchumi, kwa matarajio kwamba sera za mageuzi ya uchumi zitatekelezwa kikamilifu. Mihimili mikuu katika utekelezaji wa sera hizo inajumuisha utekelezaji wa MKUKUTA na Mpango wa "Tanzania Mini-Tiger 2020", Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo, Mkakati wa Kuendeleza Sekta Binafsi, MKURABITA na mikakati mingine. Majedwali Na. 2(a) – (c) yanaonyesha mwenendo wa ukuaji kutoka 1998-2005 na matarajio ya ukuaji katika kipindi cha 2006-2009.

Jedwali 2 (a): Pato la Taifa Kisekta (kwa bei za mwaka 1992), 1996-2005

Sh. Mil.

	1996	1997	1998	1999	2000	2001	2002	2003	2004	2005
Kilimo	708741	726098	739942	770509	796513	840275	882106	917395	970378	1020497
Uchimbaji Madini na Mawe	20579	24097	30700	33488	38144	43293	49787	58749	67798	78443
Bidhaa za Viwandani	111894	117489	126887	131491	137809	144647	156219	169653	184218	200797
Umeme na Maji	23977	24514	25870	26874	28454	29297	30200	31688	33123	34815
Ujenzi	54868	74361	65187	70866	76818	83494	92679	102872	113994	127533
Uuzaji wa Jumla, Rejareja na Mahotelini	218105	229010	239830	254114	270567	288718	308928	329009	354726	383814
Mawasiliano na Uchukuzi	71597	60079	79755	84403	89515	95154	101244	106294	112648	119833
Fedha, Bima, Mali na Huduma za Kibiashara	139058	149762	158089	164568	172291	177911	186485	194711	203222	213961
Uendeshaji wa Serikali na Huduma Nyingina	111473	115007	118114	122207	126567	130987	136307	141880	147950	155490
Toa Ushuru wa Huduma za Benki	-58581	-72327	-78548	-81229	-82359	-84418	-86781	-89819	-93541	-98104
Jumla ya Pato la Taifa GDPfc	1401711	1448089	1505826	1577291	1654319	1749358	1857174	1962432	2094516	2237079
GDPfc (fiscal year)	1995/96	1996/97	1997/98	1998/99	1999/00	2000/01	2001/02	2002/03	2003/04	2004/05
	1373479	1424900	1476957.5	1541558.5	1615805	1701838.5	1803266	1909803	2028474	2165798

Jedwali 2 (b): Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa 1996-2005

Sekta	1996	1997	1998	1999	2000	2001	2002	2003	2004	2005
Kilimo	3.90%	2.40%	1.90%	4.10%	3.40%	5.50%	5.00%	4.00%	5.80%	5.20%
Uchimbaji Madini na Mawe	9.60%	17.10%	27.40%	9.10%	13.90%	13.50%	15.00%	18.00%	15.40%	15.70%
Bidhaa za Viwandani	4.80%	5.00%	8.00%	3.60%	4.80%	5.00%	8.00%	8.60%	8.60%	9.00%
Umeme na Maji	11.10%	2.20%	5.50%	3.90%	5.90%	3.00%	3.10%	4.90%	4.50%	5.10%
Ujenzi	7.60%	35.50%	-12.30%	8.70%	8.40%	8.70%	11.00%	11.00%	10.80%	11.90%
Uuzaji wa Jumla, Rejareja na Mahotelini	3.50%	5.00%	4.70%	6.00%	6.50%	6.70%	7.00%	6.50%	7.80%	8.20%
Mawasiliano na Uchukuzi	1.10%	-16.10%	32.80%	5.80%	6.10%	6.30%	6.40%	5.00%	6.00%	6.40%
Fedha, Bima, Mali na Huduma za Kibiashara	0.40%	7.70%	5.60%	4.10%	4.70%	3.30%	4.80%	4.40%	4.40%	5.30%
Uendeshaji wa Serikali na Huduma Nyingine	1.60%	3.20%	2.70%	3.50%	3.60%	3.50%	4.10%	4.10%	4.30%	5.10%
GDPfc	4.20%	3.30%	4.00%	4.70%	4.90%	5.70%	6.20%	5.70%	6.70%	6.80%
GDPfc (Mwaka wa fedha)	1995/96	1996/97	1997/98	1998/99	1999/00	2000/01	2001/02	2002/03	2003/04	2004/05
	3.90%	3.70%	3.70%	4.40%	4.80%	5.30%	6.00%	5.90%	6.20%	6.80%

Jedwali 2(c) Pato Halisi na Makisio ya Matumizi, Kwa bei za Miaka Husika, 1996-2009

GDPmp (calendar)	1998	1999	2000	2001	2002	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009
	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Hailisi	Halisi	Halisi	Halisi	Makisio	Makisio	Makisio	Makisio
	5571255	6432911	7268380	8274607	9445483	10686333	12365503	14209092	15950274	17884803	20128720	22696239
	18.50%	15.50%	13.00%	13.80%	14.20%	13.10%	15.30%	11.70%	12.10%	12.40%	12.80%	13.00%
GDPmp (fiscal)	1997/98	1998/99	1999/00	2000/01	2001/02	2002/03	2003/04	2004/05	2005/06	2006/07	2007/08	2008/09
	5137357	6002083	6850645.5	7771493.5	8860045	10065908	11521688	13287298	15079683	16917539	19006762	21412479
	21.30%	16.80%	14.10%	13.40%	14.00%	13.60%	14.60%	15.30%	13.50%	12.20%	12.30%	12.70%

Chanzo: Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji

Mwenendo wa Bei

11. Baada ya kufikia kiwango kidogo cha asilimia 4.0 Januari 2005, kasi ya upandaji bei iliendelea kupanda na kufikia asilimia 6.5 Machi, 2006. Kwa wastani, mwaka 2005 kasi ya upandaji bei ilikuwa asilimia 4.3 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2004. Kuongezeka kwa kasi ya upandaji bei mwaka 2005 kulitokana na kupanda kwa bei za bidhaa, hususan chakula na mafuta ya petroli ambayo pia yalichangia kuongezeka kwa gharama za usafirishaji na umeme. Uhaba wa chakula katika nchi jirani za Malawi na Zambia ulichangia kwa kiasi uhaba wa chakula katika baadhi ya mikoa kwani vilisafirishwa kwenda nchi jirani.





Mapato na Matumizi ya Serikali

Mapato

12. Mwaka 2005/06, serikali ilipanga kukusanya mapato ya sh. 2,066.8 bilioni, sawa na asilimia 14.3 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na makusanyo halisi ya asilimia 13.8 mwaka 2004/05 .Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2005/06, mapato ya ndani yalifikia sh. 1,013.8 bilioni, sawa na asilimia 99.1 ya makisio ikilinganishwa na sh. 869.9 bilioni mwaka 2004/05, sawa na ongezeko la asilimia 16.5. Kati ya mapato hayo, mapato kutokana na kodi yalikuwa sh. 935.3 bilioni na mapato yasiyo ya kodi sh. 78.6 bilioni.

13. Mapato hayo ni sawa na wastani wa sh. 169.0 bilioni kwa mwezi ikilinganishwa na sh.145.0 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2004/05.

14. Kufikia Machi, 2006 mapato ya ndani yalikuwa sh. 1,544.4 bilioni ikilinganishwa na sh. 1,314.5 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2005. Mapato hayo ni sawa na wastani wa sh. 171.6 bilioni kwa mwezi ikilinganishwa na

sh.146.0 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2005. Ingawa mapato ya ndani yalikuwa chini ya makisio, kwa ujumla kumekuwepo na ongezeko la mapato ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Kuongezeka kwa mapato kulitokana na kuendelea kuimarika kwa usimamizi katika ukusanyaji kodi.

15. Mwaka 2005/06, misaada na mikopo, ikijumuisha misamaha ya madeni ilikadiriwa kufikia sh. 1,725 bilioni, sawa na asilimia 41 ya bajeti ya Serikali. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2005/06, serikali ilipokea misaada ya sh. 621.5 bilioni, ikiwa ni pungufu kwa asilimia 3.0 ya matarajio kwa kipindi hicho. Kati ya hizo. sh. 294.9 billion sawa na asilimia 47.5 zilikuwa kwa ajili ya programu ambapo sh. 192.4 bilioni, sawa na asilimia 31.0 zilikuwa za miradi. Kiasi cha sh.98.4 bilioni au asilimia 15.8 ya misaada hiyo ilikuwa kwa ajili ya mfuko wa pamoja wa nchi wahisani (basket support) wakati sh. 35.2 bilioni sawa na asilimia 5.7 zilikuwa ni misaada kwa ajili ya Mpango wa Kusaidia Nchi Maskini Zenye Madeni Makubwa (HIPC). Aidha, serikali ilipokea mikopo ya sh. 417.0 bilioni, sawa na asilimia 96.2 ya matarajio ya sh. 433.6 bilioni kwa kipindi hicho. Kati ya mikopo hiyo, sh. 253.9 bilioni ni kwa ajili ya programu, sh. 190.1 billion kwa ajili ya miradi na sh. 25.4 bilioni kwa ajili ya mfuko wa pamoja wa nchi wahisani. Katika kipindi hicho, sh. 52.4 bilioni zilitumika kulipia deni la nje.

16. Kufikia Machi 2006, fedha zilizotolewa kwa ajili ya mfuko wa pamoja wa nchi wahisani zilikuwa sh. 123.8 bilioni ikilinganishwa na matarajio ya sh. 196.6 bilioni, wakati mikopo na misaada ya programme ilikuwa sh. 548.8.bilioni, ikilinganishwa na makisio ya sh. 584.8.bilioni, sawa na upungufu wa asilimia 0.1. Wafadhili wengi waliitikia vyema mwito wa kupitisha misaada yao katika mfumo wa bajeti ya serikali.

Matumizi

17. Sera za serikali za matumizi katika mwaka 2005/06 zililenga katika kuendeleza na kuboresha usimamizi wa matumizi ili kufikia malengo ya MKUKUTA ya kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Ukiwa ni mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa MKUKUTA, Serikali ilipanga kutumia sh. 4,035.1 bilioni, sawa na asilimia 28.9 ya Pato la Taifa. Kati ya hizo, sh. 2,649.9 bilioni zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh. 1,385.2 kwa matumizi ya maendeleo. Mgawanyo wa matumizi ya kawaida yalikuwa kama ifuatavyo: Sh. 681.9 bilioni, sawa na asilimia 25.7 kwa ajili ya mishahara; matumizi mengine sh. 1,580.8 bilioni, sawa na asilimia 59.7; na Mfuko Mkuu wa Serikali ukijumuisha

ulipaji wa madeni na riba ulitengewa sh. 212.4 bilioni, sawa na asilimia 8.0 ya matumizi ya kawaida.

18. Katika nusu ya mwaka 2005/06, matumizi ya Serikali yalifikia sh. 2,122.9 bilioni sawa na asilimia 104 ya makisio ya sh. 2,038.6 au asilimia 52.6 ya bajeti ya mwaka. Kati ya hizo, sh. 1,401.1 bilioni zilikuwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 5.9 juu ya makisio ya sh. 1,323.3 bilioni. Matumizi ya maendeleo katika kipindi hicho yalifikia sh. 720.5 bilioni, yakiwa juu ya makisio kwa asilimia 0.8 au asilimia 34.0 ya matumizi yote ya maendeleo. Kufikia Machi 2006, matumizi ya Serikali yalifikia sh. 3,180.5 bilioni, sawa na asilimia 100.3 ya makisio ya bajeti ya sh. 3,171.1 bilioni ya mwaka 2005/06.

19. Kwa ujumla, kuongezeka kwa matumizi ikilinganishwa na makisio katika kipindi husika kulichangiwa hasa na mambo manne yakijumuisha, (i) ruzuku iliyotolewa kwenda TANESCO kuzalisha umeme kutokana na mitambo inayotumia mafuta ili kukabiliana na tatizo la umeme lililotokana na ukame ulioathiri sehemu nyingi nchini. (ii) kulipia gharama zilizotokana na kuahirishwa kwa Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2005 (iii) ruzuku iliyotolewa ili kununua chakula kukabili uhaba ulitokana na ukame katika maeneo mengi ya nchi na (iv) kuendelea kupanda kwa bei ya bidhaa za petroli katika soko la dunia. Serikali ilitumia dola 42 milioni, sawa na asilimia 0.3 ya Pato la Taifa kununua chakula ili kupunguza tatizo la chakula katika maeneo yaliyokabiliwa na uhaba wa chakula. Fedha za matumizi hayo ya ziada katika bajeti ya serikali zilitokana na mikopo kutoka benki, na hivyo kuathiri malengo ya ujazi wa fedha na mikopo ya ndani.

Deni la Taifa

20. Hadi Desemba 2005, deni la taifa lilifikia dola 9.96 bilioni ikilinganishwa na dola 9.73 bilioni Desemba 2004, sawa na ongezeko la asilimia 2.4. Kufuatana na taratibu zinazokubalika kimataifa, uchambuzi kuhusu uwezo wa kuhimili deni la nje umeonyesha kuwa deni hilo linahimilika. Kati ya deni hilo, dola 7.93 bilioni ni deni la nje, sawa na asilimia 79.7 ya deni lote ikilinganishwa na dola 8.02 bilioni mwishoni mwa Desemba, 2004, sawa na upungufu wa asilimia 1.1. Upungufu huo ulitokana na juhudi za serikali za kulipa deni la nje na msamaha wa madeni uliotolewa na wahisani mbalimbali chini ya utaratibu wa kuzipunguzia madeni nchi maskini duniani zenye madeni makubwa na utekelezaji thabiti wa Mkakati wa Taifa wa Madeni.

21. Uchambuzi wa mgawanyo wa madeni kwa aina ya mkopaji unaonyesha kuwa Serikali ndiyo mkopaji mkuu, ikiwa na deni la dola 5.79 bilioni (asilimia 85.9) ikifuatiwa na sekta binafsi dola 0.49 bilioni (asilimia 7.2) na mashirika ya umma dola 0.47 billion (asilimia 6.9). Kwa upande mwingine, deni la ndani lilikuwa dola 2.03 billion, sawa na asilimia 20.4 ya deni lote la taifa.

22. Kufikia mwishoni mwa Desemba 2005, deni la ndani lilikuwa dola 2.03 bilioni (sawa na sh. 2,369 bilioni), sehemu kubwa ya deni hilo ilikuwa dhamana za Serikali zenye thamani ya sh. 1,675.8 bilioni, sawa na asilimia 99.0 ya deni lote la ndani. Wanunuzi wakuu wa dhamana za serikali walikuwa ni benki za biashara, mifuko ya pensheni na Benki Kuu kwa asilimia 44.9, 24.8 na 17.6 ya deni lote la ndani kwa mtiriko huo.

Ujazi wa Fedha na Karadha

Ujazi wa Fedha

23. Katika mwaka ulioishia Juni 2005, ujazi wa fedha uliongezeka kupita kiwango kilichopangwa cha asilimia 24 kwa tafsiri pana (M_2)[1] na tafsiri pana zaidi (M_3). Ujazi wa M_2 uliongezeka kwa asilimia 27.5 ikilinganishwa na asilimia 19.2 Juni 2004 , wakati ujazi wa M_3 uliongezeka kwa asilimia 25.5 ikilinganishwa na asilimia 18.0 Juni, 2004.

Katika kipindi kilichoishia Desemba 2005, M_2 iliongezeka kwa asilimia 36.9, ikiwa ni kiwango cha juu kidogo ya makadirio ya asilimia 35.4 kwa kipindi hicho ikilinganishwa na asilimia 19.2 Desemba 2004. M_3 iliongezeka kwa asilimia 38.2 Desemba 2005, ikilinganishwa na asilimia 19.3 Desemba 2004, kiwango ambacho pia kilikuwa juu ya lengo la asilimia 34.6. Hata hivyo, kuongezeka kwa kiwango cha ujazi wa fedha kulienda sambamba na mahitaji ya fedha za kuendeshea shughuli za kiuchumi. Ongezeko hilo lilitokana zaidi na kuongezeka kwa: amana katika mabenki ; mikopo ya mabenki kwa sekta binafsi ; misaada kutoka kwa wafadhili kusaidia bajeti ; na kuongezeka kwa matumizi ya Serikali kulikosababishwa na kuahirishwa kwa Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2005, ruzuku ya Serikali kwenda TANESCO na ununuzi wa chakula. Majedwali 3(a) – (b) yanaonyesha mwenendo wa ujazi wa fedha na karadha (1998-2005).

[1] *M_0 ni fedha zilizo kwenye mzunguko nje ya benki; ; M_1=M_0 + amana za hundi; M_2 = M_1 + amana za muda maalum + amana za akiba;*
M_3 = M_2 + amana za fedha za kigeni (foreign deposits)

Jedwali 3(a): Mwenendo wa Ujazi wa Fedha na Ukuaji wa Karadha

	Kipindi kilichoishia Juni							2004 Kuishia Des.	2005 Kuishia Des.
	1998	1999	2000	2001	2002	2003	2004		
Ujazi wa Fedha –Tafsiri Finyu Zaidi(M0) banks	272667	279872	339928	375045	429384	473704	590,441.0	664,148.0	843,157.43
Amana za Hundi	208975	229122	261303	316210	386192	507444	595,622.1	651,591.3	915,652.79
Ujazi wa fedha –tafsiri finyu (M_1)	481642	508994	601231	691255	815576	981148	1186063.1	1315739.3	1,758,810.2
Amana za Muda Maalumu	132735	152902	152291	171598	218602	246720	269132.9	276396.4	422,269.39
Amana za akiba	155803	168805	203021	236184	299346	330918	401130.3	458750.2	627,168.02
Ujazi waFedha –Tafsiri Pana(M_2)	770180	830701	956543	1099037	1333524	1558785	1856326.3	2050885.9	2,808,247.6
Amana za Fedha za kigeni	177214	204193	302471	373868	464366	647109	746608.5	797234.07	1,126,738.94
Ujazi waFedha –Tafsiri Pana Zaidi (M3)	947394	1034894	1259014	1472905	1797890	2205894	2602934.8	2848120.1	3,934,986.6
Akiba Halisi ya Mali za Kigeni	410228	472304	707352	1001412	1293645	1871286	2134182.7	2379909.2	2,407,311.8
Amana Halisi Nchini	537127	539395	551662	471490	750102	710283	962910.4	932533.2	2,136,881.4
Karadha Nchini	438343	570411	696536	647342	684920	858204	1,123,597.8	1,012,357.6	1,838,844.68
Mikopo kwa Serikali	239665	314109	383098	268920	202879	199679	157606.9	(47719.74)	413,782.38
Mikopo kwa Sekta Isiyo Serikali	198678	256302	313438	378422	482041	658525	965980.9	1060077.31	1,425,062.30
Amana Halisi Nyinginezo	98784	-31016	-144875	-175852	65181	-147921	-160687.4	-79824.29	298,036.76

Jedwali 3(b): Viwango vya Ukuaji wa Karadha na Ujazi wa Fedha (Asilimia)

	Kipindi kilichoishia Juni							2005 Kuishia – Des
	1999	2000	2001	2002	2003	2004	2005	
Ujazi waFedha –Tafsiri Finyu Zaidi[2]	2.60	21.50	10.30	14.50	10.3	24.64	24.47	27.00
Amana za Hundi	9.60	14.00	21.00	22.10	31.40	17.38	33.28	40.00
Ujazi wa fedha –tafsiri finyu (M1) [3]	5.70	18.10	15.00	18.00	20.30	20.89	28.89	33.70
Amana za Muda Maalumu	15.20	-0.40	12.70	27.40	12.90	9.08	22.14	52.80
Amana za akiba	8.30	20.30	16.30	26.70	10.50	21.22	26.88	36.70
Ujazi waFedha –Tafsiri Pana ((M_2) [4]	7.90	15.10	14.90	21.30	16.90	19.09	27.48	36.90
Akiba Halisi ya Mali za Kigeni	15.20	48.10	23.60	24.20	39.40	15.38	20.54	41.30
Ujazi waFedha-Tafsiri Pana zaidi (M_3) [5]	9.20	21.70	17.00	22.10	22.70	18.00	25.49	38.20
Akiba Halisi ya Mali za Kigeni	15.10	49.80	41.60	29.20	44.70	14.00	6.80	1.20
Amana Halisi Nchini	0.40	2.30	-14.50	59.10	-5.30	35.57	56.92	129.10
Karadha Nchini	30.10	22.10	-7.10	5.80	25.30	12.20	33.86	81.60
Mikopo kwa Serikali	31.10	22.00	-29.80	-24.60	-1.60	-21.07	81.87	-967.10
Mikopo kwa Sekta Isiyo Serikali	29.00	22.30	20.70	27.40	36.60	46.69	26.23	34.40
Amana Halisi Nyinginezo	-131.40	367.10	21.40	-137.10	-326.90	8.63	-104.38	-473.40

Mikopo ya Benki za Biashara Katika Sekta Mbalimbali

24. Kufikia Desemba 2005, mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwenda sekta binafsi iliongezeka na kufikia asilimia 34.4 ikilinganishwa na asilimia 29.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2004. Ongezeko hilo lilitokana hasa na kuongezeka kwa idadi ya wateja wanaokopesheka na ambao wamekuwa wakinufaika na viwango maalumu vya makubaliano vinavyotolewa na benki; kuongezeka kwa ushindani katika sekta ya benki; kuwepo na skimu ya kuwadhamini wauzaji bidhaa nje ya nchi; na juhudi za Serikali zinazoendelea za kuboresha mazingira ya biashara. Kuongezeka kwa utoaji mikopo kwenda sekta mbalimbali kumeibua shughuli nyingi za kiuchumi na hasa katika sekta za uchimbaji madini,ujenzi, utalii, bidhaa za viwandani, biashara na kilimo. Jedwali Na. 4, linaonyesha mikopo ya benki za biashara kwa sekta mbalimbali katika mwaka 2005.

Jedwali Na. 4: Mikopo ya Benki za Biashara kwa Sekta Mbalimbali 2005 (Wakopaji Wakuu)

Sekta	Bidhaa za Viwandani	Biashara	Kilimo	Usafirishaji	Ujenzi na Majengo	Utalii	Utawala wa Umma	Madini	Nyinginezo
Sh. (bilioni)	3,222.6	3,467.1	1,990.4	1,241.4	632.3	411.2	182.8	240.3	2,892.1
Asilimia	22.60	24.3	13.80	8.20	4.40	2.90	1.3	1.7	20.3

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Maendeleo katika Soko la Fedha

Soko la Hisa la Dar es Salaam

25. Hadi Desemba mwaka 2005, makampuni nane yalikuwa yameorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam, mawili kati ya hayo yakiwa ya ni kigeni. Idadi ya makampuni hayo yamekuwa yakiongezeka kutokana na utekelezaji wa mageuzi ya kiuchumi na sekta ya fedha ambayo kwa kiasi kikubwa yameboresha mazingira ya biashara katika soko la mitaji. Jedwali Na. 5 linaonyesha makampuni yaliyoorodheshwa katika soko la Hisa la Dar es Salaam.

Jedwali Na. 5: Makampuni Yaliyoorodheshwa Katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (hadi - Desemba 2005)

Jina	Ticker	Sekta
Kampuni ya Bia Tanzania	TBL	Vinywaji
Kampuni ya Sigara Tanzania	TCC	Tumbaku
Tanzania Tea Parkers Limited	TTP/TATEPA	Kilimo
Tanzania Oxygen Limited (TOL)	TOL	Gesi na Mafuta
DAHACO	Swiss port	Usafirishaji
Kampuni ya Bia ya Afrika Mashariki	EABL	Vinywaji
Kampuni ya Saruji ya Tanga	SIMBA	Bidhaa za Ujenzi
Shirika la Ndege la Kenya	KA	Usafirishaji

Chanzo: Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE)

Mwenendo wa Viwango vya Riba

26. Mwaka 2005, viwango vya riba katika soko la fedha la ndani viliongezeka kutokana na utekelezaji wa sera za fedha za kuthibiti ujazi wa fedha. Wastani wa kiwango cha riba za amana za akiba kinachotolewa na benki za biashara uliongezeka kidogo na kufikia asilimia 2.61 Juni 2005 kutoka asilimia 2.40 Juni 2004 na ulibakia asilimia 2.60 mwishoni mwa Desemba 2005. Wastani wa kiwango cha riba za muda maalum uliongezeka kidogo kutoka asilimia 4.35 Juni 2004 hadi asilimia 4.41 Juni 2005 na kuongezeka zaidi hadi asilimia 5.20 Desemba 2005. Aidha, wastani wa kiwango cha riba cha muda maalumu (miezi 12) ulikuwa asilimia 7.7 Desemba 2005 ikilinganishwa na asilimia 5.8 Desemba 2004. Wastani wa kiwango cha riba za amana uliongezeka kutoka asilimia 3.5 Desemba 2004 hadi asilimia 3.9 Desemba 2005. Wastani wa viwango vya riba za amana zilizotolewa kwa wateja maalumu uliongezeka kutoka asilimia 8.8 Desemba 2004 hadi asilimia 10.6 Desemba 2005. Benki nyingi za biashara zimehodhi kiasi kikubwa cha amana, hivyo kutokuwepo motisha kwa benki hizo kuweza kuvutia wateja kuweka akiba katika benki hizo.

27. Viwango vya riba ya mikopo vinavyotozwa na Benki Kuu kwa benki za biashara viliongezeka kutoka wastani wa asilimia 12.60 Juni 2004, hadi asilimia 13.90 Juni 2005, na viliongezeka zaidi na kufikia asilimia 18.3 Desemba 2005. Wastani wa kiwango cha riba za hawala za Hazina uliongezeka kutoka asilimia 7.8 Juni 2004 hadi asilimia 9.3 Juni 2005, na kuchapuka zaidi hadi asilimia 14.8 Desemba 2005, wakati viwango vya riba vya papo kwa papo baina ya benki iliongezeka zaidi na kufikia asilimia 5.1 Juni 2005, kutoka asilimia 3.6 mwaka Juni 2004, na kuongezeka zaidi na kufikia asilimia 5.97 Desemba 2005.

28. Kwa jumla viwango cha riba ya mikopo vilivyotolewa na benki za biashara vilionyesha mwenendo mchanganyiko. Wastani wa jumla wa viwango cha riba ya mikopo vilivyotozwa na benki za biashara uliongezeka kutoka asilimia 14.2 Juni 2004 hadi asilimia 15.5 Juni 2005 na kuendelea kushuka kidogo hadi asilimia 15.0 Desemba 2005. Wastani wa viwango vya riba kwa mikopo ya muda mfupi, uliongezeka kutoka asilimia 15.70 Juni 2004 hadi asilimia 16.10 Juni 2005, na kushuka hadi asilimia 15.65 Desemba 2005, wakati wastani wa viwango vya riba za mikopo ya muda wa kati (miaka 2-3) ulishuka kutoka asilimia 16.2 Juni 2005 hadi asilimia 14.52 Desemba 2005. Wastani wa viwango vya mikopo ya muda mrefu uliongezeka hadi asilimia 13.9 Juni 2005 kutoka asilimia 13.1 Juni 2004, na kuongezeka kidogo hadi asilimia 14.10 Desemba 2005. Wastani wa viwango vya riba za amana zilizotolewa kwa wateja maalumu uliongezeka kutoka asilimia 9.40 Juni 2004 hadi asilimia 10.00 Juni 2005 na kuongezeka zaidi hadi asilimia 11.10 Desemba 2005. Tofauti kati ya viwango vya riba za mikopo na za amana iliongezeka na kufikia asilimia 12.2 Juni 2005, kutoka asilimia 11.50 Juni 2004, na kupungua hadi asilimia 11.04 Desemba 2005.

Kielelezo 3:Mwenendo wa Riba za Amana na Mikopo: 1998 - 2005 (kuishia Juni)



Viwango vya Riba kwa Fedha za Kigeni

29. Wastani wa viwango vya mikopo uilipungua kidogo na kufikia asilimia 8.04 Juni 2005 kutoka asilimia 8.4 Juni 2004 na ulikuwa asilimia 8.03 Desemba

2005. Wastani wa viwango vya riba za amana ya akiba ulishuka kutoka asilimia 0.9 Juni 2004 hadi asilimia 0.7 Juni 2005 na kuongezeka hadi asilimia 0.8 Desemba 2005. Kiwango cha riba kwa amana za muda maalumu kiliongezeka kutoka asilimia 1.1 Juni 2004 hadi asilimia 1.7 Juni 2005 na kuongezeka zaidi na kufika asilimia 1.9 Desemba 2005.

30. Mwaka 2005, wastani wa thamani ya shilingi ya Tanzania ilipungua hadi sh. 1,132.2 kwa dola moja ya Marekani ikilinganishwa na wastani wa sh. 1,053.3 kwa dola moja ya Marekani mwaka 2004. Aidha , thamani ya shilingi kwa dola moja ya Marekani ilifikia sh. 1,165.51 mwishoni mwa Desemba, 2005 ikilinganishwa n a sh. 1,043.0 kwa dola kipindi kama hicho mwaka 2004.



31. Katika kipindi kilichoishia Desemba 2005, kiasi cha fedha za kigeni kilichobadilishwa katika Benki kilikuwa dola 814.7 milioni ikilinganishwa na dola 711.3 milioni Desemba mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 14.5. Kutokana na mahitaji makubwa ya fedha za kigeni hususan dola za kimarekani katkika nusu ya pili ya mwaka 2005, Benki Kuu iliuza jumla ya dola za Kimarekani 3.35 milioni katika soko la fedh za kigeni. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za kukuza mitaji, shughuli za kiuchumi na pia mafuta ya petroli kwa ajili ya uzalishaji umeme.

32. Akiba ya fedha za kigeni ilipungua kutoka dola 2,296.1 milioni mwaka 2004 hadi dola 2,048.4 milioni mwaka 2005, sawa na thamani ya kuagiza bidhaa na huduma kwa miezi 6.4 ikilinganishwa na miezi 8.2 mwaka 2004. Upungufu wa akiba ya fedha za kigeni ulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kigeni ili kuagiza bidhaa za kukuza mitaji kukidhi ongezeko la shughuli za kiuchumi na pia kuagizia mufuta ya petroli kwa ajili ya uzalishaji umeme.

Mikopo Midogo

33. Benki Kuu iliendelea na jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mikopo Midogo. Ili kushirikisha wananchi wengi katika kupata mikopo ndani ya mfumo wa sekta ya fedha, mfuko ujulikanao kama "Financial Sector Deepening Trust" ulianzishwa mwaka 2004. Aidha, shughuli za kutayarisha mfumo wa kuratibu na kusimamia taasisi zinazotoa mikopo nchini ulikamilika.

Sekta ya Nje

34. Mwaka 2005, mwenendo wa sekta ya nje ulikuwa wa kuridhisha, ukiambatana na kuongezeka kwa thamani ya mauzo nje kwa bidhaa asilia na zisizo asilia. Thamani ya mauzo ya bidhaa nje iliongezeka kwa asilimia 13.8 kutoka dola 1,473.1 milioni mwaka 2004 na kufikia dola 1,676.3 milioni mwaka 2005.

35. Thamani ya mauzo ya bidhaa asilia iliongezeka na kufikia dola 354.5 milioni mwaka 2005 kutoka dola 297.8 milioni mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 19.1. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya kahawa, tumbaku na pamba. Hata hivyo, kiasi cha mauzo ya korosho nje kilipungua kwa kiasi kikubwa kutokana na kuongezeka kwa korosho zinazonunuliwa na kubanguliwa humu nchini. Kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia kulichangiwa na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa na matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo na madawa ya kuulia wadudu na mbolea.

36. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia iliongezeka na kufikia dola 1,321.8 milioni mwaka 2005 kutoka dola 1,175.3 milioni mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 12.5. Mauzo ya dhahabu ndiyo yaliyochangia kwa kiasi kikubwa ambapo thamani ya mauzo ya dhahabu ilikuwa dola 655.5 milioni ikilinganishwa na dola 629.4 milioni mwaka 2004. Ongezeko hilo lilitokana na kupanda kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji uliotokana na kuanza uzalishaji katika mgodi mpya wa dhahabu wa Tulawaka. Thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani na bidhaa nyingine pia

iliongezeka kutokana na ukarabati unaoendelea na uanzishwaji wa viwanda vipya ambao umeongeza uuzaji nje wa nguo, viatu, bidhaa za plastiki na chuma. Pamoja na mafanikio hayo, mapato yatokanayo na mauzo nje yamekuwa na uwezo wa kugharimia asilimia 63.0 tu ya uagizaji nje.

Jedwali 6: Thamani, Kiasi na Bei za Bidhaa Muhimu Zilizouzwa nje, 2001 - 2005

	2001	2002	2003	2004		Badiliko (%)
					2005_p	2004 - 2005
Bidhaa asilia:						
Kahawa						
Thamani (US$ mill.)	57.1	35.2	50	49.8	74.3	49.2
Kiasi (‘Tani 000)	48.39	36.4	46.2	38.6	46.1	19.20
Bei (US$ kwa tani)	1179.1	968.4	1,081.70	1,289.60	1.613.60	25.12
Pamba						
Thamani (US$ mill.)	33.7	28.6	46.5	74.6	111.5	49.46
Kiasi (‘Tani 000)	36.8	33.3	46.9	77.6	112.9	45.40
Bei (US$ kwa tani)	915.3	859.4	992	961.1	987.9	2.79
Katani						
Thamani (US$ mill.)	6.7	6.6	7.3	7.2	7.3	0,90
Kiasi (‘Tani 000)	13.9	12.7	13.9	12	9.3	-22.20
Bei (US$ kwa tani)	482	516.4	523.5	602.8	781.7	29.68
Chai						
Thamani (US$ mill.)	29	29.6	24.8	30.1	25.6	-14.8
Kiasi (‘Tani 000)	23	24.3	21.2	24.3	21.8	-10.50
Bei (US$ kwa tani)	1264.4	1217.8	1,170.30	1,237.30	1,178.00	-4.79
Tumbaku						
Thamani (US$ mill.)	35.7	55.5	39.9	57.6	80.8	40.10
Kiasi (‘Tani 000)	18.7	25.4	18.3	27.2	31.1	14.50
Bei (US$ kwa tani)	1906.2	2188.6	2,177.00	2,119.40	2593.1	22.30
Korosho						
Thamani (US$ mill.)	56.6	46.6	41.8	68.1	46.6	-31.57
Kiasi (‘Tani 000)	95	79	65.1	83.6	62	-25.90
Bei (US$ kwa tani)	595.4	589.7	641.6	814.2	751.1	-7.70
Karafuu						
Thamani (US$ mill.)	12.3	4	10.3	10.3	8.5	-1748
Kiasi (‘Tani 000)	2.5	1	5.6	4.3	3	-31.80
Bei (US$ kwa tani)	5026.8	4164.4	1,845.20	2,367.30	2863.5	20.96
Jumla Ndogo	231.1	206.1	220.5	297.8	354.5	19.10
Bidhaa zisizoasilia: (US$ mill.)						
Madini	302.2	383.8	552.2	680.2	711.3	4.57
Dhahabu	254.1	341.1	502.8	629.4	655.5	4.10
Almasi	27.1	22	28.6	26	24.4	-6.10
Madini mengine	21.1	20.7	20.7	24.8	31.4	26.70
Bidhaa za viwandani	56.2	65.9	83.8	110.1	156.1	41.78
Samaki na mazao ya samaki	96.8	116.8	136.2	125.7	147.5	17.40
Mauzo ya mboga na maua	11	10.9	13.7	14.3	18.3	28.10
Bidhaa nyingine zilizouzwa nje	79.2	119.2	122.9	108.1	161.5	49.50
Jumla ndogo	620.2	773.5	995.7	1,175.30	1,321.80	12.5
Jumla Kuu (US$ mill.)	**851.3**	**905.5**	**1,129.20**	**1473.1**	**1676.3**	**13.79**

Chanzo: Benki Kuu



37. Mwaka 2005, mapato yatokanayo na huduma yaliongezaka na kufikia dola 1,199.0 milioni kutoka dola 1,117.4 milioni mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 7.3. Ongezeko hili lilichangiwa na kuongezeka kwa huduma za usafiri na usafirishaji, sambamba na kuongezeka kwa shughuli za utalii na kuimarika kwa miundombinu.

38. Thamani ya bidhaa zilizoagizwa toka nje mwaka 2005 ilifikia dola za Marekani 2,661.8 milioni kutoka dola za Marekani 2,339.7 milioni mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 13.8. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za ukuzaji mitaji na bidhaa za kati kutokana na kukua kwa shughuli za uzalishaji viwandani, uchimbaji madini na utalii. Aidha, uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji uliongezeka kwa asilimia 25.4, bidhaa za kati asilimia 16.5, ambapo bidhaa za walaji zilipungua kwa asilimia 1.7.

Jedwali 7: Bidhaa Muhimu Zilizoagizwa Toka Nje, 2001- 2005

US $ Mil.

Aina ya Bidhaa	2001	2002	2003	2004	2005	Badiliko (%) 2004 - 2005
Bidhaa za Ukuzaji Mitaji	739.7	721.1	814.8	860	1078.1	25.35
Vifaa vya Usafiri	189.8	218.3	233.5	229	289.6	26.46
Ujenzi wa Mjengo	144	134.7	166.3	185.5	257.2	38.65
Mitambo	406	368.3	415.1	445.5	531.3	19.26
Bidhaa za Kati	440.8	423	679.5	712.9	830.2	16.50
Uagizaji wa Mafuta	220.7	194.8	403.3	431.8	511.2	18.39
Mbolea	15.5	20.1	28.5	54.1	64.6	19.50
Malighafi za Viwanda	204.6	208	247.7	227	254.4	12.07
Bidhaa za Matumizi ya Kawaida	534.2	516.6	630.3	764.7	751.3	-1.70
Vyakula	169.4	147.3	182.5	248.8	168.4	-32.30
Bidhaa Nyingine za Kawaida	364.8	369.3	447.9	515.9	583.0	13.00
Jumla Kuu (F.O.B)	**1560.5**	**1511.3**	**1,933.50**	**2,339.70**	**2661.8**	**13.80**

Chanzo: Banki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Mipango, Uchumi na uwezeshaji

39. Uagizaji wa huduma uliongezeka kutoka dola 965.5 milioni mwaka 2004 hadi dola 1,163.7 milioni mwaka 2005, sawa na ongezeko la asilimia 20.5. Ongezeko hilo lilitokana hasa na kuongezeka kwa malipo kwa ajili ya ujenzi, gharama za usafirishaji zilizoambatana na kuongezeka kwa uagizaji nje, safari na huduma za Serikali.

40. Mwaka 2005, urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya dola 985.5 milioni ikilinganishwa na nakisi ya dola 866.6 milioni mwaka 2004, wakati urari wa biashara ya huduma ulipungua kutoka ziada ya dola 151.9 milioni mwaka 2004 hadi ziada ya dola 35.2 milioni mwaka 2005. Urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali uliendelea kuporomoka kutoka nakisi ya dola 246.5 milioni mwaka 2004 hadi nakisi ya dola 606.1 milioni mwaka 2005. Upungufu huu ulitokana na kuagiza bidhaa nyingi kutoka nje ukilinganisha na mauzo nje. Aidha, kulikuwa na upungufu katika uhamishaji mali mwaka 2005 ikilinganishwa na mwaka 2004. Urari wa malipo yote ulikuwa na nakisi ya dola 437.5 milioni mwaka 2005 ikilinganishwa na ziada ya dola 43.4 milioni mwaka 2004.

Jedwali Na. 9: Mizania ya Malipo na Nchi za Nje, 2001 – 2005

US $ Mil.

	2001	2002	2003	2004	2005
	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Matarajio
Urari wa Bidhaa	**-709**	**-531.8**	**-717.3**	**-866.6**	**-985.5**
Zilizouzwa Nje	851.3	979.6	1,216.10	1,473.10	1676.3
Zilizonunuliwa Toka Nje	1560.3	1511.3	1,933.50	2,339.70	2661.8
Urari wa Huduma	**264.9**	**287.6**	**222.1**	**151.9**	**35.2**
Mapato	649.7	632.5	725.7	1117.4	1199
Matumizi	914.6	920.1	947.8	965.5	1163.7
Urari wa Mapato na Vitega Uchumi	**-188.5**	**-150.1**	**-162.6**	**-177.8**	**-237.1**
Mapato	55.3	67.9	87.1	81.8	79.7
Matumizi	243.8	218.1	249.7	259.6	316.9
Urari wa Uhamisho	**395.3**	**416.6**	**546.9**	**646.1**	**581.3**
Iliyoingia	474.8	477.9	609.9	711.1	656.3
Iliyotoka	79.5	61.3	63	65	74.9
Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho mali	**-237.4**	**-22.3**	**-111**	**-246.5**	**-606.1**
Urari wa Uhamisho wa Mitaji	361.5	355.4	358.2	293.6	504.9
Iliyoingia	361.5	355.4	358.2	293.6	504.9
Iliyotoka	0	0	0	0	0
Urari Katika Uwekezaji	**-353.7**	**191.6**	**257.3**	**382.8**	**46.4**
Uwekezaji Katika Hisa	467.2	429.8	526.8	469.9	325
Uwekezaji Katika Miradi	8.2	2.2	2.7	2.4	2.5
Uwekezaji Aina Nyingine	-829.1	-240.4	-272.2	89.5	281.1
Makosa na Masahihisho	580	-681.6	-449.6	-386.6	-382.7
Urari wa MalipoYote	**-809.6**	**-112.4**	**-54.9**	**43.4**	**-437.5**
Kuziba Nakisi	**809.6**	**112.4**	**54.9**	**-43.4**	**437.5**
Akiba ya Fedha za Kigeni	-182.6	-372.4	-508.8	-258.4	247.7
SDR na Mikopo	15.6	26	-2.9	-33.8	-50.5
Madai Maalum	976.2	458.8	456.8	248.8	240.3

Chanzo: Benki kuu ya Tanzania na Wizara ya Mipango,Uchumi na Uwezeshaji

Jumuiya ya Afrika Mashariki

41. Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo kama ilivyokubaliwa katika Mkataba wa kuanzisha Jumuiya. Utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo ilifanyika kama

ilivyokuwa imepangwa. Utekelezaji wa Itifaki ya Ushuru wa Pamoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulianza rasmi Januari 2005. Kufuatia kuanza utekelezaji wa Itifaki hiyo, nchi wanachama zimeanza kukekeleza marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha. Viwango hivyo ni asilimia 0, 10 and 25. Usimamizi wa utekelezaji wa Umoja wa Forodha uko chini ya Makamishina wa Forodha wa nchi wananchama.

42. Kuhusu hatua za kuunda Shirikisho la Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi wanachama, walikubaliana kuendelea na mashauriano na wadau katika kila nchi husika, kwa lengo la kufikia muafaka wa kitaifa kuhusu suala hilo. Maeneo makuu ya shirikisho ni umoja wa forodha na soko la pamoja. Kuundwa kwa Shirikisho la Jumuiya ya Afrika Mashariki kutategemea uanzishwaji na utekelezaji wa soko la pamoja ambalo hadi sasa bado halijaanza. Katika mwaka 2005, Mfuko wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulizinduliwa. Mfuko huo unalenga kugharimia shughuli za programu na miradi katika ngazi ya kikanda kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi wanachama.

Mpango Mpya wa Ushirikiano wa Kuleta Maendeleo Afrika

43. Mwaka 2001, Viongozi Wakuu wa Afrika waliidhinisha Mpango Mpya wa Ushirikiano wa Kuleta Maendeleo Afrika kama mpango wa pamoja wa kuondoa umaskini na kuongeza ukuaji wa uchumi endelevu. Tanzania, kama mwanachama wa Umoja wa Afrika, ni sehemu na inaridhia na malengo na misingi ya Mpango huo. Vile vile, Tanzania hushiriki kikamilifu na kwa manufaa katika masuala yote muhimu yaliyoainishwa katika mada kuu tano, ambazo ni: hali ya kuwa na maendeleo endelevu; kuweka vipaumbele vya kisekta; kuongeza rasilimali; ushirikiano na kujiunga na utaratibu wa nchi kujitathmini na kujipima zenyewe.

Kujiunga na Mpango wa Afrika wa Kujitathmini na Kujipima Zenyewe

44. Chini ya Mpango Mpya wa Ushirikiano wa Kuleta Maendeleo Afrika, Utaratibu wa nchi Kujipima na Kujitathmini Yenyewe (APRM) ulianzishwa. Mpango huu unatoa utaratibu au fursa kwa nchi kujiamini na kujipima au kupimwa utendaji wake na nchi nyigine, taasisi zilizoteuliwa au kundi la wataalamu. Lengo la Mpango huu ni kuzisaidia nchi zinazotathminiwa katika kuboresha uandaaji wa sera zake, kuiga utendaji mzuri, kukubaliana na viwango vilivyowekwa, misingi, taratibu na kanuni nyingine zilizokubaliwa. Pia, Mpango huu unasaidia nchi kujenga kujiamini kuhusiana na sera na mikakati imara na inayotabirika.

Hadi Januari 2005, nchi 23 ikiwemo Tanzania zilikuwa zimeridhia Utaratibu wa Nchi Kujipima na Kujitathmini Yenyewe. Tanzania iliridhia Mpango huo Februari 2005 na tayari ilikuwa imewasiliana na Sekretarieti ya APRM kwa uamuzi na utayari wake wa kutaka kufanya tathimini ya mafanikio ya uchumi wake. Serikali tayari imeshawasiliana na taasisi nne za utafiti na kupewa kibali cha kufanya utafiti juu ya utawala bora katika maeneo ya demokrasia na siasa, utawala bora na usimamizi wa uchumi, "Corporate Governance"; na maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

45. Mwaka 2005, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika iliadhimisha miaka 25 (1980-2005) tangu kuanzishwa, ambapo nchi wanachama waliendelea kutekeleza malengo na dira ya pamoja inayolenga kusukuma kanda kwenda kwenye mafanikio makubwa kupitia ushirikiano wa kikanda.

46. Nchi wananchama ziliendelea kutekeleza sera thabiti za uchumi jumla na biashara zilizolenga katika ukuaji wa uchumi endelevu, ambao utachangia katika kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya wananchi katika kanda. Matokeo yake ni kwamba, kiwango cha ukuaji wa uchumi kikanda kilikuwa asilimia 4.1 mwaka 2004, ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2003, wakati biashara miongoni mwa nchi wananchama iliongezeka kutoka kiwango kidogo cha asilimia 5.0 mwaka 1980 hadi asilimia 25.0 mwaka 2005.

Maendeleo ya Sekta Binafsi

47. Mwaka 2005, Serikali iliendelea na juhudi zake za kukuza sekta binafsi kwa kujenga mazingira bora ya uwekezaji na biashara. Utayarishaji wa Mkakati wa Maendeleo ya Sekta Binafsi utakaoongoza sekta hiyo unaendelea.

48. Serikali iliendelea na juhudi za kuboresha mazingira ya biashara na kupunguza vikwazo katika kufanya biashara kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA). MKUMBITA unalenga katika kuondoa vikwazo katika kanuni, taratibu na utawala; kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa sekta binafsi; kuboresha usuluhishi wa migogoro kibiashara; kuongeza na kuendeleza ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi. Benki ya Dunia iliunga mkono Programu ya MKUMBITA kwa kutoa SDR[6] 65 milioni kwa ajili ya Mradi wa Kiushindani wa Sekta Binafsi., ambao uliidhinishwa na Bodi ya Utendaji Desemba 2005.

49. Kupitia Programu ya MKUMBITA, Muswada wa Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara uliandaliwa na kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza Julai 2005 na unatarajiwa kuwasilishwa tena Bungeni Oktoba, 2006. Mara itakapopitishwa kuwa sheria kamili itabatilisha Sheria ya Leseni ya Biashara ya mwaka 1972, na hivyo kufuta mfumo wa sasa wa utoaji leseni na usajili. Sheria mpya ya usajili itaharakisha urasimishaji wa shughuli za biashara, ukusanyaji wa takwimu, wakati huo huo ikitoa mazingira yatakayorahisisha maafikiano na usajili wa hiari. Mageuzi ya kisheria katika kazi, ardhi, utoaji wa leseni za biashara na masuluhisho ya migogoro ya kibiashara yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, taratibu za kuendeleza MKUMBITA Zanzibar zimekamilika.

50. Programu ya MKUMBITA imepata mafanikio makubwa katika kutoa fursa kwa sekta binafsi kuchangia katika mchakato wa mageuzi ya sera na sheria kwa kuchochea na kuendeleza ari ya ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi, hivyo kuwepo umiliki na wajibu kwa sekta zote.

51. Serikali inaandaa Mradi wa Biashara Ndogo na Kati unaolenga kukuza sekta binafsi yenye ushindani mkubwa kwa kupunguza gharama za kufanya biashara. Vile vile, Mradi unalenga katika kuongeza uwezo wa sekta binafsi ya ndani kushiriki kikamilifu katika soko la ndani na la kimataifa. Mradi una maeneo matatu ambayo ni uimarishaji wa mazingira ya biashara, uendelezaji wa biashara, na kuboresha upatikaji wa huduma za mikopo. Mwongozo wa utekelezaji wa Mradi ulikamilika. Utoaji wa vitambulisho vya Taifa utatoa mchango katika ukuaji wa sekta ya biashara ndogo na kati, na kuongeza upatikanaji wa mikopo.

52. Mwaka 2005, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kiliidhinisha jumla ya miradi 550 yenye thamani ya sh. 1,651,053 milioni ikilinganishwa na miradi 454 yenye thamani ya sh. 1,246,040 milioni mwaka 2004. Kati ya miradi hiyo, miradi 339 ilikuwa mipya na 211 ilikuwa ya upanuzi na ukarabati. Miradi hii ilikuwa na uwezo wa kutoa fursa za ajira 55,663. Sekta ya viwanda iliendelea kuongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya miradi iliyoidhinishwa na ya pili katika fursa za ajira. Hata hivyo, sekta ya kilimo ambayo ina fursa nyingi zaidi za ajira ilikuwa na miradi michache iliyoidhinishwa katika mwaka huo. Kwa ujumla, kuongezeka kwa uwekezaji kulitokanana na kutengamaa kwa uchumi jumla na juhudi za Serikali katika kutekeleza mageuzi ya kisheria na kimuundo yanayolenga kusaidia ukuaji wa sekta binafsi. Jedwali 10 linaonyesha miradi iliyoidhinishwa kuanzia mwaka 1995 hadi mwaka 2005.

Jedwali 10: Miradi iliyoidhinishwa (1995 – 2005)

Mwaka	Miradi iliyoidhinishwa	Miradi ya wawekezaji wa ndani	Miradi ya wawekezaji wa nje	Miradi ya ubia	Jumla ya ajira	Thamani Tshs. (milioni)
1995	82	35	20	27	11,304	186,829
1996	111	49	17	45	19,745	376,979
1997	199	90	53	56	37,311	602,642
1998	213	111	46	56	35,010	447,275
1999	181	81	43	57	12,933	399,138
2000	1624	745	343	536	241,250	4,957,288
2001	220	87	53	80	24,699	1,091,805
2002	311	126	104	81	33,132	1,024,536
2003	372	155	109	108	198,458	1,669,363
2004	454	208	119	127	56,057	1,246,040
2005	550	281	131	138	55,663	1,651,063
Total	**4,317**	**1,968**	**1038**	**1,311**	**725,562**	**13,652,958**

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

Uwekezaji wa Mitaji ya Kigeni ya Moja kwa Moja

53. Katika miaka mitano iliyopita, Uwekezaji wa Mitaji ya Kigeni ya Moja kwa Moja Tanzania umekuwa ukiongezeka kwa wastani wa dola za Kimarekani 443.74 milioni kutoka mwaka 2001 hadi 2005. Utafiti kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Kigeni ya Moja kwa Moja uliofanywa mwaka 2004 na Benki Kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Kituo cha Uwekezaji Tanzania ulibainisha kuwa zaidi ya asilimia 72.5 ya wawekezaji waliridhika na mazingira ya uwekezaji nchini. Uwekezaji wa mitaji ya moja kwa moja kutoka nje ilikuwa na thamani ya dola za Kimarekani 469.9 milioni mwaka 2004 ikilinganishwa na dola za Kimarekani 526.8 milioni mwaka 2003. Kuongezeka kwa uwekezaji wa mitaji ya moja kwa moja mwaka 2003 kulitokana na uwekezaji mkubwa katika sekta ya madini. Mwaka 2005, thamani ya uwekezaji wa mitaji ya moja kwa moja kutoka nje ilikadiriwa kufikia dola za Kimarekani 325.0 milioni. Kupungua kwa thamani ya uwekezaji kulitokana na kupungua kwa uwekezaji katika sekta ya madini. Jedwali namba 11 linaonyesha mwenendo wa uwekezaji wa mitaji ya moja kwa moja kutoka nje katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005. Mapitio yaliyofanywa katika takwimu za uwekezaji wa mitaji ya moja kwa moja kutoka nje ilikuwa ni kutaka kujua uwekezaji halisi wa moja kwa moja uliopo nchini ikilinganishwa na kumbukumbu zilizoko katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

Jedwali 11: Mwenendo wa Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje (1995 – 2005)

Mwaka	1995	1996	1997	1998	1999	2000	2001	2002	2003	2004	2005
Thamani ya Uwekezaji (dola milioni)	150.86	148.64	157.8	172.2	516.7	463.4	467.2	430	526.8	469.9	325

Chanzo: Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwekezaji, Benki Kuu ya Tanzania

54. Katika jitahada za kukuza uwekezaji nchini, miswaada miwili ya sheria iliwasilishwa Bungeni Februari 2006. Mswada wa kwanza ulikuwa wa kufanya marekebisho ya Sheria ya mwaka 2002 ya Kanda za Usindikaji wa Bidhaa za Kuuza Nje, ambayo ilianzisha Mamlaka ya Kanda za Usindikaji wa Bidhaa za Kuuja Nje. Mswada wa pili ulikuwa wa kuanzisha Sheria ya mwaka 2006 ya Kanda Maalum za Kiuchumi.

Urekebishaji na Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma

55. Hadi Desemba 2005, jumla ya mashirika 323 na mali za mashirika 625 yalikuwa yamebinafsishwa tangu Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma ilipoundwa. Mashirika na mali za mashirika hayo yalinunuliwa na wawekezaji wa ndani, wawekezaji wa nje na ubia kati ya wawekezaji wa ndani na nje kwa njia ya hisa, uuzaji wa mali, ukodishaji na ufilisi.

56. Mwaka 2005, jumla ya mashirika 136 yalibinafsishwa, ikijumuisha uuzaji wa mashirika ya umma 10 na mali za mashirika zipatazo 126, ikilinganishwa na uuzaji wa ujumla ya mashirika 172, uliyojumuisha mashirika 26 na mali za mashirika zipatazo 146 mwaka 2004. Moja ya shughuli kubwa ya ubinafsishaji iliyofanyika mwaka 2005 ni makubaliano ya uuzaji wa asilimia 49 ya hisa za NMB kwa shirikisho la makampuni lililoongozwa na Rabobank Nederland ya Uholanzi, ambayo yalitiwa saini tarehe 30/09/2005 kati ya Serikali na shirikisho liliwakilishwa na Rabobank.

57. Ubinafsishaji wa Shirika la Reli Tanzania ulikamilishwa tarehe 10/03/2006 baada ya kampuni ya M/s RITES kutoka India kushinda zabuni ya kuendesha Shirika hilo, kazi itakayoanza Augusti 2006.

58. Hadi mwezi Machi 2006, kulikuwa na mashirika 36 ambayo yalikuwa katika hatua mbalimbali za ubinafsishaji. Ubinafsishaji wa Kampuni ya Ugavi wa Umeme Tanzania uliahirishwa kutokana na uchangamano, unyeti na umuhimu wake katika maendeleo ya uchumi na jamii. Changamoto katika sekta ndogo ya umeme ni kuongeza uwezo wa kuzalisha na kuweza kutoa huduma ya umeme kwa asilimia 90 ya watu, ambao kwa sasa hawapati huduma hiyo. Hata hivyo, sekta binafsi haitegemewi kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika uzalishaji, na usambazaji wa umeme. Ubinafsishaji wa Kampuni ya Uvuvi Tanzania utafanywa na Wizara ya Mali Asili na Utalii. Baadhi ya mashirika yanayosubiri taratibu za ubinafsishaji ni

pamoja na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia, sehemu ya kibiashara ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (ukiondoa Kitengo cha Makontena ambacho kilishakodishwa), Shirika la Bima la Taifa, Kampuni ya Huduma za Meli katika maziwa na mashirika mengine ambayo utaratibu wa ubinafsishaji haujaanza au yamewekwa chini ya mfilisi baada ya mwekezaji kushindwa kuwekeza katika mashirika hayo kwa muda uliokubaliwa.

Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania

59. Utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) ulianza mwaka 2005/06. MKUKUTA unalenga katika matokeo na ushirikiano miongoni mwa sekta zote na una nguzo tatu muhimu, nazo ni ukuaji wa uchumi na kupungua kwa umaskini wa kipato; ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na utawala bora na uwajibikaji. Baada ya kufanya mapitio ya Mfumo wa Ufuatiliaji Umaskini wakati wa utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini (MKU) (2000-2004) na kuzingatiwa katika MKUKUTA (2005-2010), mfumo mpya uliandaliwa ambao unaitwa Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA, ukiwa unajumuisha timu tatu za wataalamu badala ya timu nne kama ilivyokuwa kwa MKU. Timu hizo ni Sensa, Upimaji na Ukusanyaji wa Takwimu; Utafiti na Uchambuzi; na Mawasiliano. Mfumo unalenga katika kutathmini utekelezaji wa MKUKUTA kama ilivyokuwa kwa Mfumo wa Ufuatiliaji Umaskini wakati wa utekelezaji wa MKU. Ili kutekeleza MKUKUTA, mipango na mikakati mbalimbali imekuwa ikitekelezwa, kama vile Mpango wa Kuharakisha Maendeleo 2020; Mkakati wa Maendeleo wa Sekta wa Kilimo, Mfuko wa Maendeleo wa Jamii, MKUMBITA, MKURABITA na Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu.

Umaskini Vijijini

60. Lengo mojawapo la MKUKUTA ni kupunguza kiwango cha umaskini kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2010 kwa kuongeza ukuaji wa uchumi na kupunguza tofauti za kipato. Kumekuwepo na mafanikio makubwa katika mwenendo wa uchumi jumla ambayo yalichangiwa kwa kiasi kikubwa na sekta ya kilimo, ambayo huajiri zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania. Kupungua kwa umaskini hutegemea kiwango cha ukuaji wa uchumi katika maeneo ya vijijini, hususan katika sekta ya kilimo. Ingawaje pamekuwepo na mafanikio makubwa katika uchumi jumla, tija katika sekta ya kilimo imebakia kuwa ya chini na hivyo kukwamisha juhudi za kupunguza umaskini vijijini.

61. Tafiti za Matumizi ya Kaya za mwaka 1991/92 na 2000/01, zinaonyesha kuwa umaskini vijijini ulipungua kidogo kwa asilimia 2.0. Aidha, Tafiti zilibainisha

kuwa mwenendo wa umaskini ulikuwa wastani wa asilimia 2.2 kwa pato la ukuaji wa sekta ya kilimo na kiwango hicho kitaendelea hadi 2010. Kutokana na mwenendo huo, lengo la MKUKUTA la kupunguza umaskini uliokithiri kwa asilimia 50 huenda lisifikiwe mwaka 2010, hivyo juhudi zaidi zinatakiwa ili kufikia lengo jumla la kitaifa la kiwango cha umaskini wa asilimia 19.0 mwaka 2010.

Jedwali 12: Mwenendo wa Halisi na Makisio wa Viashiria vya Umaskini 2001 – 2010[7]

	1991	2001	2002	2003	2005	2006	2006	2007	2008	2009	2010	Lengo 2010
Vijijini	40.8	38.6	36.8	36.1	34.5	32.9	31.1	30.3	28.8	27.6	26	**20**
Mijini	28.4	23.1	20.8	18.6	17.1	15.3	14.1	12.7	11.5	10	8.8	**14**
Kitaifa	38.6	35.6	33.7	32.7	31.1	29.5	28	26.8	25.4	24.2	23.1	**19**

Chanzo: PHDR 2005

Ilibainishwa pia kwamba, kushuka kwa umaskini kuna uhusiana mkubwa na kukua kwa uchumi, hivyo mkakati unatakiwa kuandaliwa ili kuhakikisha kiwango cha juu cha ukuaji wa uchumi kinapatikana katika kipindi hicho, na kuhakikisha kiwango cha ukuaji wa sekta ya kilimo hakipungui asilimia 6.0 kwa mwaka.

Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara

62. Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) unalenga katika kuwezesha kurasimisha rasilimali na biashara kutoka mfumo usio rasmi kwenda katika sekta rasmi. Mpango huu unatarajia kuweka mfumo wa kisheria wa rasilimali na biashara ambao utawawezesha wananchi kurahisisha na kuwahamasisha kuthaminisha rasilimali asili zao na kukuza uchumi huria katika utawala wa sheria na kuongeza kipato binasfi au cha makundi. Mpango utatekelezwa kwa awamu nne, ambazo ni: upembuzi yakinifu, kupanga mifumo mbalimbali; utekelezaji na ukuzaji rasilimali na utawala bora.

63. Tathmini ya sekta isiyo rasmi ambayo ilifanyika kati ya mwezi Novemba 2004 na Septemba 2005, ilibainisha kwamba sekta hiyo ilikuwa na rasilimali halisi zenye thamani ya dola za Kimarekani 29.3 bilioni, ambapo dola 2.9 bilioini na dola 26.4 bilioni zilikuwa biashara zisizo halali na rasilimali zisizohamishika kwa mtiririko huo. Aidha, asilimia 98 ya shughuli za biashara na asilimia 89 ya mali zote zilikuwa sio rasmi. Mpango uko katika hatua ya pili ya utekelezaji ambayo inategemewa kukamilika Juni 2006.

III. MASUALA MUHIMU YA KISERA YALIYOJITOKEZA MWAKA 2005/06

64. Katika mwaka 2005/06, masuala muhimu ya kisera yaliyobainishwa kuwa agenda ya kipaumbele katika kipindi cha muda wa kati ujao ni: kasi ya ukuaji wa uchumi; uwekezaji katika miundombinu; urekebishaji mishahara ya watumishi na kuongeza tija, utekelezaji wa MKUKUTA, utafiti na maendeleo; kuongeza ajira; na utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mageuzi na Maboresho ya Sekta ya Fedha.

Ukuaji wa Uchumi

66. Kasi ya ukuaji wa uchumi katika viwango vya juu na endelevu inahitajika ili kuweza kupunguza umaskini wa kipato na kuongeza ubora wa maisha ya wananchi. Ili kufikia lengo hili, juhudi zaidi na endelevu zitaelekezwa katika maeneo yafuatayo:

(i) Kuendeleza na kuimarisha mageuzi ya sera za kiuchumi na kijamii;
(ii) Kupanua wigo wa mapato ya ndani;
(iii) Kuboresha sekta ya kilimo, hasa kilimo cha umwagiliaji na kuwa na mfumo wa uzalishaji mifugo na uvuvi wa kisasa zaidi;
(iv) Kuongeza ufanisi katika sekta ya masoko na ushirika;
(v) Kuendelea kujenga mazingira yatakayovutia wawekezaji kutoka nje na ndani ili kuwekeza katika kanda maalum za kiuchumi zitakazozalisha bidhaa na huduma, hususan katika sekta za kilimo, utalii, viwanda na maliasili;
(vi) Kuhimiza uwekaji wa akiba na uwekezaji;
(vii) Kuelekeza rasilimali zaidi katika maeneo yanayochangia kwa haraka ukuaji wa uchumi kama vile sekta za kilimo, miundo mbinu, viwanda na nishati;
(viii) Kukuza na kuimarisha biashara za kikanda na za kimataifa kwa kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma za kuuza nje kwa kuzingatia viwango na ubora wa kimataifa;
(ix) Kuendelea kutekeleza MKURABITA;
(x) Kuendelea kutekeleza MKUMBITA;
(xi) Kuhamasisha utumiaji wa mfumo wa utengenezaji wa kundi na mfululizo wa ongezeko la thamani; (***cluster formation and value addition chain)****; na*

(xii) Kuendeleza shughuli za uzalishaji na biashara ndogo na za kati (SMEs) vijijini na mijini ili kukuza uzalishaji na kuongeza ajira kwa wananchi.

67. Ili kupunguza mzigo wa deni la nje, juhudi zaidi za kusimamia uchumi na kuongeza uzalishaji kwa kutumia rasilimali zilizopo zinahitajika. Aidha, Serikali itaongeza juhudi zaidi katika kukusanya mapato ya ndani kwa kupanua wigo wa mapato utakaowezeshwa na utekelezaji wa MKURABITA, MKUMBITA, utoaji na utumiaji wa vitambulisho vya Taifa na upimaji na utoaji wa hati miliki.

Marekebisho ya Sekta ya Umma

68. Sehemu muhimu ambayo imekuwa ikitatiza utekelezaji wa marekebisho ya sekta ya umma ni urekebishaji wa mishahara ya watumishi wa umma kwa miaka mingi. Matokeo yake ni kwamba watumishi wengi wa umma wenye ujuzi na uzoefu wamekuwa wakiacha kazi na kutafuta maslahi mazuri katika sekta binafsi, hivyo kuathiri utoaji wa huduma za umma kwa ufanisi zaidi. Ili kuongeza tija na ufanisi zaidi katika utoaji huduma za umma na kuhakikisha kuwa watumishi wenye ujuzi na uzoefu wanabakia katika utumishi wa umma, Serikali itaendelea kutekeleza marekebisho ya mishahara. Aidha, Serikali itapitia upya taratibu na programu za mafunzo ya watumishi wa umma.

69. Ili kuimairisha madaraka katika mamlaka za serikali za mitaa, juhudi zaidi zinahitajika kulenga katika kuwezesha mamlaka za serikali za mitaa katika kuboresha upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo, ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu, ufuatiliaji na usimamizi wa mapato na matumizi. Ukamilishaji wa usambazaji wa Mfumo Tungamanishi wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) katika mamlaka za serikali za mitaa utaongeza usimamizi wa fedha za Serikali.

Maendeleo ya Kilimo

70. Kilimo kinaendelea kuwa tegemeo kuu la Uchumi wa Tanzania. Hata hivyo, sekta hii inakabiliwa na matatizo ya kilimo cha umwagiliaji kisichoendelezwa, mitaji midogo, huduma duni za ugani, miundombinu hafifu vijijini, wanyama na wadudu waharibifu wa mazao na magonjwa mbalimbali ya mazao, teknolojia duni na kilimo cha kutegemea mvua. Pia, sekta inakabiliwa na tatizo la kuyumba kwa bei katika soko la dunia na utaratibu usioridhisha wa masoko katika baadhi ya maeneo na kiwango kidogo cha muunganiko na sekta nyingine za uzalishaji.

71. Ili sekta ya kilimo iweze kukua katika kiwango cha juu na endelevu, jitihada zitaelekezwa katika;

(i) kuanzisha mfumo wa kisasa wa kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji wa mifugo;
(ii) kuboresha miundombinu ya kilimo;
(iii) kuhimiza usindikaji wa mazao na kupanua kilimo kwa kuzalisha mazao anuwai ya kilimo;
(iv) kuhakikisha kuwa kuna upatikanaji wa huduma bora za ugani;
(v) Kuboresha taratibu za upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima; na
(vi) Kuboresha upatikanaji wa masoko, ikiwemo kiwango bora cha habari juu ya masoko.

Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

72. Juhudi za ukusanyaji mapato ya ndani zilizokadiriwa kufikia uwiano wa asilimia 13 ya Pato la Taifa, ulikuwa juu kidogo ya uwiano wa nchi ya Uganda ambao ulikuwa asilimia 13.4, lakini ulikuwa chini ya ule wa nchi ya Kenya wa asilimia 22.8 ya Pato la Taifa. Aidha, asilimia 59 ya matumizi yote yaligharimiwa na fedha za ndani, ikiwa chini kidogo ikilinganishwa na nchi za Kenya na Uganda ambapo ilikadiriwa kufikia asilimia 60.

73. Serikali itaendelea kutekeleza mageuzi ya mfumo wa kodi, ikiwemo kuimarisha utawala na usimamizi katika Idara ya Forodha. Pia Idara ya walipa Kodi Wakubwa itaimarishwa zaidi na ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na kodi utaboreshwa. Aidha, Serikali itatekeleza mradi wa Taifa wa utoaji wa vitambulisho na upimaji ardhi na utoaji wa hati miliki.

Ujazi wa Fedha na Karadha

74. Wakati Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kusimamia ukwasi katika uchumi kwa kutumia sera ya fedha, Serikali kwa upande wake itaimarisha utekelezaji wa sera za bajeti na fedha zinazolenga katika kuendeleza kutengamaza uchumi na kukuza uchumi. Hata hivyo, pamoja na kuongezeka kwa mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi**,** tatizo lililobaki ni la kimuundo katika sekta ya fedha, ambalo linasababisha kuwepo kwa vikwazo au mashaka kwa benki za biashara kutoa mikopo. Pia, Serikali imeendelea na utaratibu wa kuuza dhamana za Serikali ikiwemo hawala za hazina na hatifungani ili kuziba nakisi ya bajeti yake na hivyo kutoa fursa kubwa kwa sekta ya benki kuendelea kuwekeza maeneo yenye dhamana za uhakika. Haya yote yamechangia kuendelea kuwepo kwa tofauti kubwa

kati ya riba za amana na mikopo kubakia juu. Ili kumaliza tatizo hilo na kuongeza upatikanaji wa mikopo kutoka benki za biashara, Serikali na Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Mageuzi na Maboresho ya Sekta ya Fedha.

Kuongeza Uwekezaji katika Miundombinu

75. Serikali imekuwa ikichukua hatua za kukuza miundombinu kwa kupitia upya maendeleo, kuainisha changamoto na njia za kugharimia shughuli na maendeleo ya miundombinu. Serikali inaendelea kubuni njia za kuboresha na kuongeza uwekezaji katika miundombinu ili kuharakisha ukuaji wa uchumi na kuondoa umaskini kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia na MKUKUTA. Kwa kuwa ujenzi wa miundombinu unahitaji rasilimali nyingi, Serikali imeainisha maeneo ya kimkakati ya kuwekeza miundombinu ambayo yana matokeo ya kuharakisha ukuaji wa uchumi. Maeneo ambayo yatapewa kipaumbele ni:

(i) Kuimarisha na kupanua miundombinu iliyopo, hususan barabara na reli;
(ii) Uwekezaji katika maeneo yenye fursa ya kilimo cha umwagiliaji, barabara na reli ili kuharakisha usafirishaji wa mazao ya kilimo;
(iii) Uwekezaji katika maeneo yenye vivutio vya kitalii;
(iv) Uwekezaji katika maeneo yenye madini;
(v) Kuendeleza na kuboresha bandari za Mtwara na Tanga na ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza; na
(vi) Uwekezaji katika barabara zinazozunguka nje ya Jiji la Dar es Salaam. Uwekezaji huo utahusisha ujenzi wa barabara ya kutoka Kimara hadi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu J.K. Nyerere; Madale-Mbezi Luisi na kuboresha barabara za Morroco-Bunju; Shekilango, Old Bagamoyo na Sam Nujoma kufikia kiwango cha njia nne.

Mazingira

76. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itasimamia, kuimarisha na kuelimisha jamii na kuhimiza ushiriki wa watu katika utunzaji na usimamizi wa mazingira. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaelekeza rasilimali za kutosha katika kuanzisha usimamizi endelevu wa maeneo yenye vyanzo vya maji na upandaji miti katika maeneo yenye miinuko. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka katika kupunguza uchafuzi wa mazingira na kuhimiza utupaji salama wa taka. Aidha, masuala yanayohusu mazingira yataendelea kuingizwa katika sera na mikakati ya sekta zote za uchumi.

Utafiti na Maendeleo

77. Utafiti na maendeleo ni kipengele muhimu katika kukuza uchumi na kuendeleza uchumi tulivu wenye uwezo wa kushindana kwa mafanikio katika ulingo wa kimataifa. Mgawanyo wa rasilimali za ndani kwa ajili ya utafiti na maendeleo katika Tanzania, unakadiriwa kuwa asilimia 0.01 ya Pato la Taifa , kiasi ambacho hakikidhi mahitaji ya utafiti na maendeleo. Aidha, uhamishaji wa teknolojia umeshindikana kutokana na kutokuwepo na uhusiano wa karibu kati ya tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti hizo. Pia hakuna ushirikiano wa kutosha na uratibu sahihi miongoni mwa wadau wakuu katika utafiti na maendeleo, hasa kati ya wafadhili, Serikali, sekta binafsi, na taasisi za kitaaluma na utafiti.

78. Ili kukuza utafiti na maendeleo kunahitajika kuongeza bajeti inayoelekezwa kwenye utafiti na maendeleo; kuongeza uwezo wa wataalamu katika masuala ya utafiti, kuhimiza matumizi mazuri ya taasisi za utafiti zilizopo nchini na kujenga uwezo wa kurekebisha na kutumia teknolijia za kigeni; na kutumia ushauri wa matokeo ya tafiti mbalimbali. Kuna haja ya kuboresha uratibu wa utafiti na maendeleo nchini ili kunufaika na matokeo ya tafiti na kuongeza ushiriki wa wahusika.

Huduma za Kijamii

79. Serikali inaendelea kutekeleza Mpango wa Pili wa Kimkakati wa Sekta ya Afya (2003-2008), unaolenga katika kuboresha utoaji huduma katika ngazi za wilaya na hospitali za rufaa. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya afya, juhudi zaidi zinahitajika kuelekezwa katika kupunguza vifo vya watoto wachanga; kupunguza vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua; vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano; udhibiti maambukizo mapya ya VVU na kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI; na udhibiti wa malaria.

80. Serikali katika juhudi zake za kuboresha mfumo wa elimu nchini, imeanzisha programu/mipango mbalimbali, ikiwemo Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES). Utekelezaji wa MMEM umeonyesha ongezeko kubwa la uandikishaji wa jumla na halisi wa watoto. Mafanikio yaliyopatikana katika elimu ya msingi yanazidi kuchochea changamoto ya kuboresha na kuendeleza elimu ya sekondari na elimu ya juu**.** Juhudi zaidi zinahitajika ili kupanua na kuboresha elimu ya juu ili kukabili changamoto za ukuzaji rasilimaliwatu na kutumia fursa zilizopo katika ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

81. Serikali kupitia Mpango wa Muda wa Kati katika sekta ya maji, imetekeleza mipango na mikakati mbalimbali sambamba na Sera ya Taifa ya Sekta ya Maji ya 2002. Hata hivyo, changamoto iliyopo ni upatikanaji wa maji safi kwa wananchi mijini na vijijini, hivyo juhudi zaidi zinahitajika katika kuongeza uwekezaji katika skimu za maji maeneo yote ya vijijini na mijini.

82. Serikali inaandaa utaratibu wa namna ya kuweza kutoa ajira 200,000 za kazi kila mwaka. Kwa wakati huu, sekta rasmi inauwezo wa kutoa ajira 30,000 za kazi kwa mwaka, wakati sekta isiyo rasmi hutoa nafasi za ajira kati ya 50,000 na 60,000 kwa mwaka. Uwekezaji katika sekta za madini, utalii na kilimo, utatoa fursa kubwa za ajira. Vile vile, mpango unaoendelea wa kukuza biashara ya uuzaji nje kwa kuanzisha Maeneo Maalum ya Kiuchumi na Kanda za Kusindika Bidhaa kwa Ajili ya Kuuza Nje ni mojawapo ya maeneo yenye uwezo wa kutoa fursa nyingi za ajira. Serikali pia inaendelea kuboresha mazingira ya biashara kwa ajili ya kukuza maendeleo ya sekta binafsi, ikiwemo kukuza shughuli za biashara ndogo na za kati na mafunzo ya ufundi ili kuongeza fursa za kujiajiri.

Mpango wa Tanzania wa Kuharakisha Maendeleo 2020

83. Mpango wa Tanzania wa Kuharakisha Maendeleo 2020 ni chombo muhimu katika kutekeleza MKUKUTA na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ambao uliandaliwa ili kuharakisha kasi ya ukuaji wa uchumi katika Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara. Mpango unatoa fursa ya kuharakisha kukuza uchumi kwa kuiga maendeleo ya kiuchumi ya Mashariki mwa Asia. Mpango huu unalenga katika kuboresha mazingira ya biashara ya kiushindani ili kuvutia wawekezaji wa mitaji ya moja kwa moja toka nje (ambao wanafananishwa na ndege wanaohama kutafuta sehemu nzuri ya kutagia mayai) na wawekezaji wa ndani kwenye Kanda Maalum za Kiuchumi. Manufaa ambayo yanatarajiwa kupatikana kutokana na Mpango huu ni pamoja na kuongezeka kwa ajira, kuenea kwa matumizi ya teknolojia, kuongezeka kwa uuzaji nje, na faida ambazo zitaongeza kasi ya kiwango cha ukuaji wa uchumi. Mpango huu unakusudia kuanzisha kanda maalum za kiuchumi zipatazo 25 nchi nzima na utaanza na miradi ya majaribio kwa kila sekta ya uchumi na kusambaza mafanikio kwa nchi nzima kwa njia ya Z-A, (yaani kutafuta masoko kwanza kabla ya uzalishaji).

84. Utekelezaji wa Mpango wa Tanzania wa Kuharakisha Maendeleo 2020 ulianza mwaka 2005/06. Programu na miradi mbalimbali zimekwisha ainishwa kwa ajili ya utekelezaji wa haraka katika kipindi cha muda wa kati, ikiwemo ujenzi wa

Benjamin William Mkapa Special Economic Zone – Mabibo, Dar es Salaam; Bio-Diesel – Arusha; Mchuchuma Coal Mine – Ludewa; Ujenzi wa ICT Science Park – Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na Programu ya Upandaji wa Misitu – Mtwara na Tanga kutegemeana na wawekezaji.

Awamu ya Pili ya Mageuzi ya Sekta ya Fedha

85. Mfumo wa fedha Tanzania unaweza kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi. Tatizo linalokabili sekta hii ni ukosefu wa nyenzo za kuwezesha utoaji wa mikopo ya muda mrefu, ikiwemo ukosefu wa utaratibu wa kimuundo na wa kisheria na pengo la kiukwasi linalolenga hasa kwenye mahitaji makubwa kutoka sekta za uzalishaji na sekta saidizi.

86. Changamoto kubwa iliyopo ni kuanzisha taasisi za kifedha zenye uwezo endelevu wa kutoa mikopo ya muda mrefu. Juhudi zaidi na endelevu zinahitajika kuelekezwa katika kuanzisha Mfumo wa kisera na kisheria; kuanisha na kutambua ukubwa wa mahitaji ya vyanzo vya nyenzo za kutoa mikopo ya muda mrefu katika sekta za uzalishaji na sekta saidizi; kuainisha na kuanzisha taratibu za kutoa mikopo ya muda mrefu; na kutayarisha mkakati wa kutatua vikwazo vilivyopo ktika upatikanaji wa mikopo na huduma nyingine za kibenki.

IV. MISINGI NA MALENGO YA UCHUMI NA MAENDELEO YA JAMII 2006/07-2008/09

87. Misingi ya malengo ya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kwa kipindi cha muda wa kati (2006/07 – 2008/09), ni kama ifuatavyo:

(i) Kuendelea kutengamaa kwa vigezo muhimu vya uchumi jumla, ikiwa ni pamoja na ukuaji wa Pato la Taifa; kasi ya upandaji bei; mapato ya ndani; na viwango vya ubadilishaji wa fedha;

(ii) Kuongezeka kwa ufanisi katika utekelezaji wa MKUKUTA, na kuelekeza rasilimali zaidi katika maeneo yatakayokuza uchumi kwa haraka katika kipindi cha muda wa kati; kama vile Kanda Maalum za Kiuchumi na Kusindika Bidhaa za Uuzaji Nje, MKURABITA na Mpango wa Tanzania wa Kuharakisha Maendeleo 2020;

(iii) Kiwango cha ukuaji wa sekta ya kilimo (mazao, mifugo,uvuvi na misitu) kinatarajiwa kushuka na kufikia asilimia 3.8 mwaka 2006 kutoka asilimia 5.2 mwaka 2005 kutokana athari za ukame mwaka 2005/06 na kuongezeka tena mwaka 2007 hadi asilimia 5.0;

(iv) Sekta za biashara ya jumla na reja reja (ikijumuisha utalii), usafirishaji na mawasiliano, na ujenzi zinatarajiwa kukua kwa kiwango cha juu mwaka 2006 kuliko ilivyokuwa mwaka 2005;

(v) Kuendeleza mageuzi ya kiuchumi na kijamii katika kipindi cha muda wa kati na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika miaka ya nyuma;

(vi) Kuendelea kuongezeka kwa mapato ya ndani kutokana na mabadiliko ya mfumo na usimamizi wa kodi, kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji na biashara rasmi, na kupanuka kwa wigo wa kodi;

(vii) Mapato ya nje, ikiwemo misaada na mikopo yenye masharti nafuu inatarajiwa kubakia katika kiwango cha mwaka 2005/06, na unafuu wa madeni chini ya mpango wa HIPC utaendelea kutolewa na nchi wahisani na mashirika ya kimataifa;

(viii) Kuendelea kukua kwa sekta binafsi, kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji wa ndani na wa moja kwa moja kutoka nje na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara nchini; na

(ix) Kuimarika kwa sera za fedha ambazo zitajionyesha katika kiwango cha chini cha mfumuko wa bei, tofauti ndogo kati ya riba za amana na mikopo ya benki na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi.

VI MALENGO NA SHABAHA YA SERA ZA UCHUMI JUMLA KATIKA MWAKA 2006/07 -2008/09

88. Malengo ya jumla ya uchumi jumla yanalenga katika kutekeleza MKUKUTA ili kufikia kiwango cha juu cha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Malengo na shabaha za sera za uchumi jumla kwa kipindi cha mwaka 2006/07 – 2008/09 ni kama ifuatavyo:

(i) Pato la Taifa halisi litakua kwa asilimia 5.9[8] mwaka 2006, asilimia 7.3 mwaka 2007, na asilimia 7.7 mwaka 2008 na kuongezeka hadi asilimia 7.9 mwaka 2009;

(ii) Kasi ya upandaji bei itapungua hadi asilimia 4.5 (kwa bei za mwaka 2001) mwishoni mwa Juni 2007, kwa kulingana na viwango vitakavyokuwepo katika nchi tunazofanya nazo biashara kwa wingi;

(iii) Kuongezeka kwa mapato ya ndani yatakayofikia uwiano na Pato la Taifa kwa bei husika kwa asilimia 14.5 mwaka 2006/07, asilimia 14.7 mwaka 2007/08, na asilimia 14.8 mwaka 2008/09;

(iv) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha (kwa tafsiri pana, M_2) litakalowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi, na kasi ya upandaji bei;

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni itakayoweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 7;

(vi) Kuwa na kiwango cha ubadilishaji wa fedha kinachopatikana katika soko, Benki Kuu ikibakia na jukumu la kupunguza na kudhibiti kupanda na kushuka kwa mzunguko wa fedha; na

(vii) Kuharakisha mageuzi katika sekta ya fedha ikijumuisha kuondoa vikwazo vya kimfumo na kimuundo ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi

V. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI NA UFUATILIAJI WA MASUALA MUHIMU YALIYOJITOKEZA NA MISINGI NA MALENGO YA SERA ZA JUMLA ZA UCHUMI NA MAENDELEO YA JAMII, 2006/07 – 2008/09

89. Mafanikio ya utekelezaji wa malengo ya mfumo wa sera za jumla za uchumi na mendeleo ya jamii unahitaji ushirikishwaji mpana zaidi na utumiaji wa rasilimali kutoka kwa wadau wote, ikiwemo Serikali kama mtekelezaji, sekta binafsi kama mbia, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi zitoazo huduma za kiraia kama washiriki hai na waungaji mkono. Kwa hiyo ni wajibu wa kila Wizara, Idara, Mkoa, na Asasi za Serikali zinazojitegemea na Serikali za Mitaa kutayarisha mipango na bajeti kwa kuzingatia mwelekeo wa misingi na malengo yaliyotolewa katika kipindi cha miaka mitatu ijayo, ili kufanikisha malengo ya kuimarisha kutengemaza uchumi; kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na ukuaji uchumi endelevu, kuboresha ustawi wa jamii, na kupunguza umaskini. Jedwali lifuatalo linaonesha utekelezaji na ufuatiliaji wa masuala muhimu ya kisera na malengo ya mfumo wa sera za jumla.

MATRIKI YA UWAJIBIKAJI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MASUALA MUHIMU YA KISERA YALIYOJITOKEZA NA MALENGO YA MFUMO WA SERA ZA JUMLA

Na.	Masuala Muhimu ya Kisera Yaliyojitokeza	Mtekelezaji Kiongozi	Mshirikishwaji	Muda wa Utekelezaji
1.	Kuendelea kutengemaza uchumi	MUU	BENKI KUU, HAZINA	2006/07 – 2008/09
2.	Kuendeleza na kuboresha sera ya kiuchumi na kijamii	MUU, HAZINA	WIZARA, IDARA, MIKOA, WILAYA, SERIKALI ZA MITAA	2006/07 – 2008/09
3.	Kupanua wigo wa mapato na kuongeza ukusanyaji mapato ya ndani	HAZINA	MUU, MAMLAKA YA MAPATO	2006/07 – 2008/09
4.	Kukifanya killimo kuwa cha kisasa zaidi	MAFSC	TAMISEMI	2006/07 – 2008/09
5.	Kujenga mazingira bora ya biashara	MUU	WIZARA, IDARA, MIKOA, WILAYA, SERIKALI ZA MITAA	2006/07 – 2008/09
6.	Kukuza na kuimarisha biashara za kikanda na kimataifa	VIWANDA	AFRICA MASHARIKI, NJE, MUU	2006/07 – 2008/09
7.	Kukuza biashara ndogo na za kati (SMEs)	VIWANDA	MUU, HAZINA, BENKI KUU, TAMISEMI, ARDHI	2006/07 – 2008/09
8.	Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa MKUKUTA	MUU	WIZARA, IDARA, MIKOA WILAYA SERIKALI ZA MITAA	2006/07 – 2008/09
9.	Utekelezaji wa MKURABITA	MUU	VIWANDA, ARDHI, TAMISEMI	2006/07 – 2008/09
10.	Kuongeza uwekezaji katika miundombinu	MUU	HAZINA, NISHATI, TAMISEMI, BENKI KUU, KILIMO ARDHI, MALIASILI, MIUNDOMBINU	2006/07 – 2008/09
11.	Kusimamia na kudhibiti deni la nje	HAZINA	MUU, BENKI KUU	2006/07 – 2008/09
12.	Utekelezaji wa Marekebisho ya Mishahara ya Watumishi wa Umma	OR-UTUMISHI	HAZINA, MUU,	2006/07 – 2008/09
13.	Upatikanaji wa ajira	KAZI	MUU	2006/07 – 2008/09
14.	Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mageuzi katika Sekta ya Fedha (SGFSR)	HAZINA	BENKI KUU, MUU TAMISEMI	2006/07 – 2008/09
15.	Utekelezaji wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa	TAMISEMI	MUU, HAZINA	2006/07 – 2008/09
16.	Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Shule za SekondaRI (MMES)	ELIMU NA MAFUNZO	TAMISEMI, HAZINA ELIMU YA JUU	2006/07 – 2008/09
17.	Upanuzi wa elimu ya Juu	ELIMU YA JUU	ELIMU NA UFUNDI, HAZINA	
18.	Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mageuzi katika Sekta ya Afya.	AFYA	TAMISEMI	2006/07 – 2008/09